REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

THIRD ASSEMBLY-SECOND SESSION

THE HANSARD

Wednesday, 6th September 2023

SPECIAL SITTING

(Convened via Kenya Gazette Notice No. 11828 of 5th September 2023)

The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 9:30 a.m.

[The Speaker (Hon. Mwambire) in the Chair]

PRAYER

COMMUNICATIONS FROM THE CHAIR

VISITING STUDENTS FROM KIZURINI SECONDARY SCHOOL

The Speaker (Hon. Mwambire)**:** Waheshimiwa, leo tumepata wageni kutoka shule ya upili ya Kizurini. Hawa ni wanafunzi wa kidato cha nne; wamekuja kusoma maswala ya Kiswahili. Katiba yetu ina tambua lugha tatu za kitaifa ambazo ni; Kiswahili, Kiingereza na lugha ya Ishara. Hivyo basi, kama mnachangia leo mnaweza kutumia lugha yotote katika lugha hizi tatu bora muweze kueleweka.

Pia, mtanisamehe kwa kuwa itabidi nisome kwa Kiingereza kuhusu mkao wetu wa leo.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

SPECIAL SITTING CONVENED VIDE GAZETTE NOTICE NO. 11828

The Speaker (Hon. Mwambire)**:** This is a Special Sitting, as you already know. It is in Gazette Notice No. 11828, and it is Pursuant to Standing Order 26 (1) of the County Assembly Standing Orders. It is notified that for the information of the Members of the County Assembly of Kilifi and the general public, the Assembly shall have a Special Sitting on Wednesday, 6th September 2023 from 9:30 a.m. to 2:30 p.m. at the County Assembly Chamber, County Assembly of Kilifi premises situated behind immigration House in Malindi Town.

The main business to be transacted shall be: -

a) Consideration of the Report of the Committee on Appointment on vetting of the nominee for the position of County Secretary;
b) Tabling and consideration of the Report of the Sectoral Committee on Devolution, Public Service and Disaster Management on the vetting of Nominees to the County Public Services Board; and
c) Tabling and consideration of the Report of the Committee on Lands, Energy, Housing and Urban Development on the Vetting of Nominees to the Malindi Municipality Board.

Dated the 4th of September 2023 and signed by the Speaker of the County Assembly as required by law.

PAPERS LAID

REPORT OF THE COMMITTEE ON APPOINTMENTS ON THE VETTING OF THE NOMINEE TO THE POSITION OF COUNTY SECRETARY AND THE HEAD OF COUNTY PUBLIC SERVICE

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Asante, Bw. Spika, kwa nafasi hii. Ningeendelea katika lugha ya Kiswahili kulingana na ugeni ambao tuko nao, watoto wetu kutoka shule ya upili ya Kizurini lakini kwa sababu *Order Paper* ambayo tuko nayo imenakiliwa katika lugha ya Kiingereza, basi nitaendelea kwa lugha hiyo. Ninawakaribisha vijana wetu katika Bunge hili.

Mr. Speaker, Sir, I beg to lay the following Report on the Table: -

Report of the Committee on Appointments on the Vetting of the Nominee to the position of County Secretary and the Head of County Public Service.

(Hon. Kombo laid the document on the Table)

REPORT OF THE DEVOLUTION, PUBLIC SERVICE AND DISASTER MANAGEMENT COMMITTEE ON THE VETTING OF NOMINEES FOR POSITIONS OF CHAIRPERSON AND MEMBERS OF THE COUNTY PUBLIC SERVICE BOARD

Hon. Zia: Asante, Bw. Spika, kwa nafasi hii. Kwa faida ya wanafunzi, jina langu naitwa mheshimiwa Samson Zia Kahindi, nikiwakilisha Wadi ya Adu. Karibuni wageni, mjisikie huru na muwe makini katika kusikiliza mjadala wetu.

Mr. Speaker, Sir, I beg to lay the following Report on the Table: -

The Report of the Devolution, Public Services and Disaster Management Committee on the Vetting of Nominees for positions of Chairperson and Members of the County Public Service Board.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

(Hon. Zia laid the document on the Table)

REPORT OF THE LANDS, PHYSICAL PLANNING AND URBAN DEVELOPMENT COMMITTEE ON THE VETTING OF NOMINEES TO THE MALINDI MUNICIPALITY BOARD

Hon. Ray: Thank you, Mr. Speaker Sir, for this opportunity. For the benefit of the visitors, I am hon. Ray Mwaro Katana, MCA (Member of County Assembly), Sokoni Ward.

I beg to lay the following Report on the Table: -

The Report of the Lands, Physical Planning and Urban Development Committee on the vetting of nominees for the position of Members of the Board for Malindi Municipality.

(Hon. Ray laid the document on the Table)

NOTICES OF MOTIONS

ADOPTION OF THE REPORT ON THE VETTING OF MR. MANGI MWARO BAYA KALUWA TO THE POSITION OF COUNTY SECRETARY AND HEAD OF PUBLIC SERVICE

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Mr. Speaker, I beg to give Notice of the following Motion: -

THAT, this House adopts the Report of the Committee on Appointments on the vetting of Mr. Mangi Mwaro Baya Kaluwa to the position of County Secretary and Head of Public Service laid on the Table of this House today Wednesday, 6th September 2023.

ADOPTION OF THE REPORT ON THE VETTING OF NOMINEES TO POSITIONS OF CHAIRPERSON AND MEMBERS OF THE COUNTY PUBLIC SERVICE BOARD

Hon. Zia: Thank you, Mr. Speaker, Sir. I beg to give notice of the following Motion: =

THAT, this House adopts the Report of the Devolution, Public Service and Disaster Management Committee on the vetting of Nominees to the positions of Chairperson and Members of the County Public Service Board laid on this House today Wednesday, 6th September 2023.

Thank you, Mr. Speaker, Sir.

The Speaker (Hon. Mwambire): Yes, Chairperson Lands, Physical Planning and Urban Development Committee.

ADOPTION OF THE REPORT ON THE VETTING OF NOMINEES TO THE MALINDI MUNICIPALITY BOARD

Hon. Ray: Thank you, Mr. Speaker, Sir. Once again, I beg to give notice of the following Motion: -

THAT, this House adopts the Report of the Lands, Physical Planning and Urban Development Committee on the Vetting of nominees to the position of Members of the Malindi Municipality Board laid on the Table of this House on Wednesday, 6th September 2023.

The Speaker (Hon. Mwambire): Clerk, next Order!

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

MOTIONS

ADOPTION OF THE REPORT ON THE VETTING OF MR. MANGI MWARO BAYA KALUWA TO THE POSITION OF COUNTY SECRETARY AND HEAD OF PUBLIC SERVICE

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Thank you very much, Mr. Speaker, Sir. I beg to move the following Motion: -

THAT, this House adopts the Report of the Committee on Appointments on the vetting of Mr. Martin Mangi Mwaro Kaluwa to the position of County Secretary and Head of Public Service laid on the Table of this House.

Bwana Spika, Kamati hii ya Uteuzi iliweza kukaa na kumhoji Bw. Martin Mwaro na wakati wa kumhoji tuliweza kupitia makaratasi yake ya elimu na pia ya shughuli alizokuwa ametenda hapo awali za kufanya kazi.

Kamati hii iliweza kuona kwamba, Bw. Mwaro alikuwa na elimu ya kutosha katika nafasi hii ama ya kumwezesha kufanya kazi hii ya *County Secretary*. Pia, tuliona kwamba Bw. Mwaro, alikuwa na ujuzi wa kutosha kufanya hii kazi kama amehujumu ama amehudumu katika Serikali Kuu kabla ya wakati wa ugatuzi akaanza kufanya kazi kama *District Officer* na akaweza kupandishwa cheo mpaka akafika ngazi ya kuwa *District Commissioner*.

Baada ya hapo, aliweza kufanya kazi katika kiwango hiki cha *County Secretary* katika Kaunti jirani ya Kwale na aliweza kufanya kazi pale kwa miaka kumi (10) na kulingana na utendaji kazi wake katika Kaunti ile jirani, tuliweza kuona kwamba alifanya kazi nzuri zaidi. Kwa kuwa yeye ni mtoto wa Kilifi, tukaona hiyo itakuwa ni kumuongezea alama katika nafasi hii ya kuwa atufanyie kazi tukiamini kwamba ataweza kutufanyia kazi nzuri kama ile ambayo aliifanya katika Kaunti Jirani. Kwa hivyo, kulingana na uamuzi wa Kamati tuliona kwamba Bw. Mwaro anafaa na ningeuliza waheshimiwa katika Bunge hili tuweze kuipitisha hii Ripoti ili Bw. Mwaro aweze kuwa *County Secretary* wa Jimbo hili letu la Kilifi. Ningetaka kumuuliza mheshimiwa Martha Koki aweze kuniunga mkono kwa jambo hili. Asanteni.

Hon. (Ms.) Koki: Naunga mkono. Naweza kuendelea kujadili?

The Speaker (Hon. Mwambire): Yes.

Hon. (Ms.) Koki: Asante, Bw. Spika, kwa nafasi hii. Kwanza, nichukue nafasi hii kwa niaba ya mheshimiwa Jonathan Birya Fondo kuwakaribisha wanafunzi wa kutoka Kizurini. Kwa wale ambao hawanijui, kwa majina naitwa mheshimiwa Martha Koki Musyoki, nikiwa shangazi yenu jirani kutoka pale Mariakani. Mheshimiwa alinipigia simu jana jioni, akaniambia kuwa mtakuwa wageni wetu na kwa sababu hajisikii vizuri hangeweza kuwa na sisi leo na akaniambia nichukue nafasi hii ya kipekee kuweza kuwakaribisha.

Kwa hivyo, kwa niaba ya mheshimiwa Jonathan Birya Fondo, kwa niaba yangu, wakaazi wa Kaloleni na wote wa Mariakani tunawakaribisha katika Bunge hili. Karibuni sana na nimesikia nyinyi ni wanafunzi wa kidato cha nne, najua mko karibu kufanya mitihani. Ingawa siku zimebakia chache, tunajua mmejitayarisha vya kutosha. Mambo ni matatu; mupite ama mupite ama mupite. Kwa hivyo, tunawaombea muweze kufanya vizuri katika mitihani yenu.

Tukirudi katika mjadala ambao tuko nao, Bw. Spika, nimesimama hapa nikiwa mmoja wa ile Kamati ambayo ilimfanyia *vetting* Mr. Martin Mwaro katika nafasi hii ya *County Secretary* kama vile mwenzangu alivyotangulia kuzungumza.

Kwanza, nipongeze Kamati yote kwa ile kazi waliyoifanya na pia nipongeze ile *secretariat* yetu ambayo tuliweza kufanya kazi hata hatukuwa na mapumziko; wengine wetu

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

wakati wa wikendi ndio wakati wa kuwa mashinani lakini tulikuwa tunafanya hii kazi ili kazi ya wakaazi wa Kilifi iweze kuendelea. Mimi kwa kibinafsi, nimemjua Martin Mwaro akiwa CS (*County Secretary)* katika Kaunti jirani na sababu ambazo zilinifanya nimjue ni kwa ule utendajikazi wake akiwa upande ule.

Nilikuwa nina ufuatilizia kwa ukaribu na nikawa namuomba Mwenyezi Mungu aweze kutujalia hata sisi siku moja katika Kaunti yetu tuweze kupata *County Secretary* kama yeye. Mbali na kumjua kwa utendakazi wake, namjua ni mcha Mungu maana kuna wakati alivyokuwa yuko Kwale tulikuwa tukishiriki katika Kanisa moja. Mkiangalia katika stakabadhi zake ni mtu ambaye amekomaa kikazi, amepanda ngazi tofauti tofauti za kikazi na kwa uhakika kama tunavyoona yanayoendelea ndani ya Kaunti yetu ya Kilifi hapa ni kazi tu. Tunajua kuwa tutakapoenda kumpitisha…

The Speaker (Hon. Mwambire): Mheshimiwa Ibrahim anaomba kuongea, kuna kitu anaona kina matatizo hebu mpatie nafasi.

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Asante, Bw. Spika. Mnenaji ambaye yuko kwenye Sakafu, ambaye amekaa chini saa hii ametuambia amemjua Martin Mwaro kwa muda mrefu na pia wamekuwa wakishiriki kanisa pamoja, lakini Bw. Spika, ningeomba aambie Bunge hili ni kanisa gani walikuwa wanashiriki. Bw. Spika, kumekuwa na utata wa makanisa, kuna la kina Pastor Ezekiel na Pastor Mackenzie ni muhimu atuambie ni kanisa gani?

Hon. (Ms.) Koki: Asante, Bw. Spika, na nakuomba kama kutatokea tena mapingamizi kama hayo ya *Majority Leader* niweze kuulizwa kama nataka kufahamishwa ama sitaki kwa sababu sikujua amesimama kwa mambo gani. Lakini kwa sababu ya wageni na nafikiri tuko katika mitandao ni kanisa la St. Peters, Mariakani ambapo saa hizi mimi ni *Mother's Union* na nafurahi kushiriki katika kanisa hilo.

Kwa hivyo, Bw. Spika, nimesimama hapa kuunga asilimia mia kwa mia kama Bunge tuweze kumpitisha Bw. Martin Mwaro ili Kaunti yetu iweze kutimia na zile *structures* ambazo zinatakikana na kazi iende mbele. Kwa sababu tumepitisha bajeti yetu ya kwanza tangu uchaguzi na hii bajeti kufanya kazi ni lazima zile ofisi zote upande ule wa *Executive* ziwe zimeweza kutimizika ndio tukaweze kufanya kazi bila kizuizi. Mimi, Bw. Spika, nimeangalia *mood* ya hili Bunge hata sioni haja ya kutoa nafasi kwa mtu mwingine, uliza swali tumalize twende kwa *Public Service Board*. Asante sana.

The Speaker (Hon. Mwambire): Na si useme unaunga mkono, si ulikuwa unaunga mkono aliyekuwa akielezea. *You are supposed to second* si ndio?

Hon. (Ms.) Koki: Yes, I second Mr. Speaker, Sir.

The Speaker (Hon. Mwambire): Kiswahili japo rahisi hususan sisi ambao tunatoka katika mwambao wa Pwani lakini kina uzito wake pia. Kuna wakati unaweza kulegeza ulimi, kuna wakati ulimi unakuwa mwepesi. Wakati nikisoma shule ya upili ya Mariakani ambayo saa hii ni shule ya upili ya wavulana ya Mariakani, nilikuwa mkwasi mkuu sana wa Kiswahili na nilikuwa katika kile kikundi cha sanaa ya Kiswahili. Tulifahamishwa kwamba kuna tofauti kubwa ya kusikia na kuhisi. Hivyo basi, yule mwakilishi wa Wadi ya Kaloleni si kuwa hasikii vizuri bali hahisi vizuri. Si kuwa amekosea lakini kuna semi na ile sanifu, ninawaambia wale ambao wataandika insha, sisi hatuandiki insha, yetu ni kuongea habari ifike, kuomba kura na mahitaji mengine. Kwa hivyo hahisi vizuri.

(Question proposed)

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Hassan: Nashukuru sana, mheshimiwa Spika, kwa kunipatia hii nafasi. Wageni karibuni, sisi kule Zanzibar tunasema *chei chei*, yaani habari ya asubuhi, sijawaambia muitikie. Sisi ndio wale magwiji wa Kiswahili lakini nisipoteze muda mrefu; yangu yatakuwa tu mafupi. Nimesimama kuunga mkono huyu ndugu yangu Mwaro kupata hii nafasi ya huu ukatibu wa Kaunti. Nafikiri nitakuwa sijakosea nikisema namuunga mkono kwa sababu hata ukitazama *file* yake inajieleza kwamba huyu mtu ni kiongozi.

Pia tukifwatilia ile mienendo yake na mikakati aliyokuwa yuko nayo katika ile Kaunti jirani kwa kweli huyu ni kiongozi anayetufaa. Tangu saa hizo, huu mwaka mzima tumeumaliza sijaona kuna tashwishwi yoyote. Kwa hivyo, mimi nasimama na ningeomba Bunge letu hili tukufu tuungane mikono kwa pamoja na tusonge mbele. Asante sana mheshimiwa, nimeshukuru. Nimesimama kuunga mkono.

Hon. (Ms.) Maneno: Asante sana, Bw. Spika. Wageni wetu wa Kizurini, karibuni. Mimi ni jirani yenu, naitwa mheshimiwa Mary Maneno Anzazi kutoka Kambe Ribe. Nataka kuwafahamisha mwanzo tu majukumu ya Bunge hili ni matatu. Yaani mambo ni matatu; kuwakilisha wananchi, kutunga sheria na uangalizi wa jinsi Kaunti inavyofanya kazi ama Gatuzi letu la Kilifi linavyofanya kazi likiwa chini ya kiongozi wetu mheshimiwa Gideon Maitha Mung'aro.

Nimesimama tena kuunga mkono Ripoti hii ambayo iko mbele yetu ili tuweze kumpitisha Bw. Martin Mangi Mwaro Baya Kaluwa. Nimeweza kupitia stakabadhi zake hasa kwa Kiswahili *CV* tunaiita mtaala; amefanya kazi nzuri akiwa jirani yetu pale Gatuzi la Kwale. Nimeangalia masomo yake, Martin Mwaro anafaa kupeleka gurudumu la Kilifi ama gatuzi mbele ili wananchi waweze kuhisi na waweze kuona yale…

The Speaker (Hon. Mwambire): Mheshimiwa Elina Mapenzi ana shauku na jambo na angependa ufafanuzi.

Hon. (Ms.) Mapenzi: Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa manufaa ya wale ambao wanatazama mimi ninaitwa Elina Mapenzi, nimesimama kama angependa mnenaji niweze kumfahamisha kitu fulani ndani ya usemi wake wa awali.

The Speaker (Hon. Mwambire): Mheshimiwa Mary, ungependa kufahamishwa?

Hon. (Ms.) Maneno: Bw. Spika, atanifahamisha baada ya Bunge. Asante.

The Speaker (Hon. Mwambire): Mheshimiwa Mapenzi, kwa sababu amekataa itabidi utue kidogo, umpatie nafasi aendelee. Mheshimiwa Mary, endelea.

Hon. (Ms.) Maneno: Kwa hivyo, mimi ninaunga na Ripoti ya Kamati…

The Speaker (Hon. Mwambire): Mheshimiwa Thaura ana swala nyeti angependa…

Hon. Thaura: Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa Hoja ya nidhamu na ninafikiri mheshimiwa ambaye yuko katika Sakafu hana uwezo wa kunizuilia kulisema lile ambalo ningehitaji kulizungumza. Nimesikia kwamba CV inaitwa mtaala, sina hakika kwamba inaitwa mtaala na aliyesimama ni mwalimu *by profession* na ninaamini kwamba analijua ninalozungumzwa kwa hivyo ninafikiria hilo angesahihisha kabla tuendelee.

(Laughter)

Hon. (Ms.) Maneno: Bw. Spika, hiyo ilikuwa ni nidhamu ama alikuwa ananijuza?

The Speaker (Hon. Mwambire): Ameuliza kuhusu nidhamu lakini nafikiria ukiangalia katika Kanuni za Bunge ni kumaanisha kwamba alikuwa anasema ni vizuri kupeeana habari ambayo inausawia kuliko kupeana habari itakuwa ni ya kukanganya Bunge. Sasa pengine ungefafanua lile swala ambalo amelielezea ili Bunge likaelewa kama kweli ni mtaala ama kuna

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

neno lengine sahihi zaidi ambalo linaweza kusaidia hata wengine wakiwa wanaongea kule. Wakati mwingine waheshimiwa huitwa sehemu tofauti tofauti.

Hon. (Ms.) Maneno: Asante Bwana Spika, kuna mambo mengi kwa mitandao anaweza pia ku *Google*. Kwa sababu naamini kwamba mheshimiwa Thaura yeye ni msanii na anaelewa hizo lugha. Kwa hivyo ningeomba…

(Loud consultations)

Mheshimiwa Spika, ningeomba nimalizie hapo na uniruhusu nikae na mimi nimeunga mkono. Asante.

(Laughter)

The Speaker (Hon. Mwambire): Kwa ufupi mheshimiwa Mary alipokuwa anaeleza kazi za Bunge ni kama kwa ufupi alikuwa anasema Bunge ni kama wanyapara wa serikali. Kwa sababu hata wakitunga sheria wanaangalia serikali kama inaitimiza vile ilivyotungwa ama kuna matatizo na iwapo kuna matatizo wanaregea wanakuja irekebisha ili iwe inaweza kuwa rahisi kutimiza yale walikuwa wamelenga.

Hon. Moses Furaha Kea, leo nitawasoma kwa majina yote matatu ili wakaazi wa Kilifi wawajue. Wengine hawajui kwamba anaitwa Moses Furaha Kea, wanajua *Milele*, sasa afadhali tumuite kwa yale majina kamili yaliyoko katika stakabadhi zake.

Hon. Kea: Asante sana, Bw. Spika, kwa kunipatia nafasi hii kuzungumza machache. Mwanzo, ningetaka kuwakaribisha vijana wetu wa Kizurini na wamefanya jambo la busara sana kwanza kufika hapa ili kujifundisha mambo yanavyoenda. Kesho, watakuwa viongozi wetu na ni vizuri sana wafahamu kile ambacho kinaendelea.

Nimesimama hapa kuunga mkono Hoja hii ya kumpitisha ndugu yangu Martin Mwaro kuwa katibu na mkuu wa Kilifi *Public Service Board*. Ni vizuri sana kama wana Kilifi tupate watu ambao wana uzoefu wa kazi.

The Speaker (Hon. Mwambire): Umesema *Public Service Board*?

Hon. Kea: Kama County Secretary halafu pia mkuu wa Kilifi …

The Speaker (Hon. Mwambire): Ielezee vile iko. Kuna tofauti kubwa na vile ulivyoelezea.

Hon. Kea: Wa Kilifi Public Service Board. Kile cha msingi ambacho nataka kueleza ni wasifu ambao ndugu yetu Martin Mwaro yuko nao kulingana na haya makaratasi yake ambayo ametupatia kujitetea ili aweze kupata hii nafasi ya kuwa kiongozi wetu. Wacha makaratasi peke yake, Bw. Spika, hata uzoefu wa kazi imekuwa jambo la muhimu sana katika kuendeleza Kilifi yetu kusonga mbele. Huyu bwana alipokuwa akifanya kazi katika serikali kuu, alipanda madaraja tofauti kwa sababu ya ueledi wake wa kazi ambao...

(Hon. Tete stood on a Point of Information)

Hon. Tete: Naomba kumfahamisha mheshimiwa ambaye yuko kwenye Sakafu …

The Speaker (Hon. Mwambire): Mheshimiwa ungependa kufahamishwa?

Hon. Kea: Hakuna neno, unajua elimu unajifundisha kila wakati, kwa hivyo akinifahamisha nitashukuru.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Tete: Asante. Hapa Bungeni tuko na wageni ambao wametutembelea na ni wanafunzi, si vijana. Ulikuwa unajaribu kutuambia kwamba tumetembelewa na vijana, sio vijana. Ni wanafunzi kutoka shule ya upili ya Kizurini na pia walimu wao.

Hon. Kea: Poleni wanafunzi kwa kuwaita vijana, lakini mwalimu wangu wa Kiswahili *Wallah Bin Wallah* alinieleza vizuri lakini hayo ni ya siku nyengine. Nasema kwamba Kilifi iko na bahati sana kupata mtu kama huyu Martin Mwaro kuwa kiongozi wetu wa kuendeleza shughuli za gatuzi letu la Kilifi. Katika serikali kuu mtu kupanda daraja kutoka sehemu moja mpaka nyengine haijakuwa rahisi, mpaka awe ana uzoefu wa kile ambacho anakifanya na huyu bwana amefanya kazi.

Mwanzo, wakati ule kabla ugatuzi kulikuwa kuna serikali kuu ambapo kulikuwa na watu wanaitwa *District Officers*; alitoka hapo kwa sababu ya kazi yake nzuri na akapanda mpaka akawa *District Commissioner*. Serikali hiyo ya kitambo haikuwa ya mchezo kikazi na huyu bwana akawa anapanda hayo madaraja kwa sababu ya ufanyakazi wake. Hata alipotoka katika Serikali Kuu na kuingia Serikali za Ugatuzi akiwa kule Kwale, hatujasikia manung'uniko yake kama watu wa Kilifi. Ikawa ni vizuri sana tupate mtu kama huyo arudi nyumbani ili aje atufanyie kazi ili sisi tutoke katika hatua tuliyo sasa mpaka hatua nyengine pale mbele.

Kuna watu hupata makaratasi kwa sababu siku hizi hii inaitwa ni Kenya na hatuhami tuko hapa; kuna vimambo hufanyika lakini ufanyaji kazi wake tumeuona na hata ninaona kwamba tumechukua muda mrefu kumuidhinisha kikamilifu kuwa kiongozi wetu kwa ile nafasi ambayo tunataka kumpatia sasa.

Heko pia kwa Kamati ambayo ilihusika ambao ni Wabunge wenzangu katika Bunge hili la Kilifi. Walikaa na kupiga msasa wakiongozwa haswa na Spika wetu ambaye alifanya kazi nzuri sana kuona kwamba hawa haswa huyu Martin Mwaro, amemuangalia vizuri sana. Siamini kwamba nimekaa na watu ambao wanafanya kitu ambacho hawakielewi. Tumpatie huyu Bw. Mwaro hii nafasi na ile kazi ambayo ameianzisha aweze kuikamilisha kikamilifu. Naunga mkono. Asante.

Hon. Emmanuel: Thank you, Mr. Speaker. May I take this opportunity to welcome all students from Kizurini Secondary School; welcome. I stand to support the Motion. I want to let this House know that I know Mr. Martin Mwaro at a personal level; he was my neighbour especially when we were in primary school. I know his history. I will not repeat what has been said but I want to give my reasons why I am supporting him to be the County Secretary and the Head of Public Service Board in this county.

One; it has come to my attention that Martin Mwaro has been serving in Kwale County for two terms and now there is an amendment to the law; I want to say that the law that brought the amendment of the limit of service for the County Secretaries in Kenya was not in the mother law in 2012, but in 2020. There was an amendment that was done that came to enforce and this law does not make or affect Mr. Martin Mwaro to serve in Kilifi County as the County Secretary because during the time of his tenure in Kwale, the law was not in force yet. So, when the time came for the law to be enforced, he had two years to accomplish his two-term limit of service and that did not affect him legally to be the Kilifi County Secretary. I wanted to make that statement because the law became effective on 27 July 2020. Thank you, so much. I stand to support the Motion.

The Speaker (Hon. Mwambire)**:** Based on the request I have before me here; I will limit Members from contributing. I know you wanted to exhibit your fluency in the languages before the students but try to go to the point while making contributions to save time; we still have two other Reports for debate.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Zia: Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii. Naunga mkono kuteuliwa kwa Bw. Martin Mwaro kuwa katibu katika gatuzi letu na pia mkuu wa utumishi wa umma. Kulingana na Wasifu wake ambao uko katika jarida hili ni kwamba huyu mtu ana uzoefu na kazi zake ambazo alikuwa akizifanya. Naomba waheshimiwa wenzangu tupitishe huyu Bwana ili afanye kazi.

Hon. Mohamed: Asante, mheshimiwa Spika. Kwa manufaa ya wanafunzi kutoka Kizurini jina langu ni mheshimiwa Mwambire Mohamed nikiwakilisha wakaazi wa Bamba; karibuni Bunge hili tukufu. Nimesimama kuungana na wenzangu ili kumpa nafasi Bw. Martin kuwa katibu mkuu katika Gatuzi hili la Kilifi. Tumekuwa tukitamani sana kupata mtu mzoefu ambaye anaweza kuchukua Kaunti hii kiwango cha jirani yetu Kwale. Naunga mkono.

Hon. Ziro: Asante sana, Bw. Spika. Kwa manufaa ya wanafunzi wa Kizurini mimi ni mheshimiwa Edward Ziro nikiwakilisha Wadi ya Mwanamwinga ambayo ni wadi jirani huko Kaloleni. Nataka kuchukua nafasi hii, kuwakaribisha katika Bunge hili. Naunga mkono uteuzi wa Bw. Martin, yeye yuko na kila kitu kinachohitajika kupeleka Kaunti hii mbele. Ukiangalia utendaji kazi wake kwa ule muda mfupi amekuwa akifanya kazi kwa niaba ya Katibu hapa Kilifi, tumeona mambo yamebadilika. Nina imani kuwa uteuzi wake utapeleka Kaunti yetu mbele.

Hon. Juma: Asante, Bw. Spika kwa nafasi hii ili nidokeze jambo kuhusiana na uteuzi huu wa Bw. Mwaro. Kwa manufaa ya wanafunzi naitwa Juma Chengo, nawakilisha Wadi ya Mnarani. Kaloleni ni kwa wajomba zangu. Pia tumuombee afueni ya haraka mheshimiwa Birya. Naunga mkono Bw. Mwaro kuwa Katibu wa Gatuzi letu la Kilifi.

Jambo lingine, alipokuwa Kwale, hiyo Kaunti ilitangazwa mshindi kwa mambo ya maendeleo. Zaidi nataka kuwajulisha kwamba mimi ni mwanahabari; tuache kuangalia makaratasi tu. Nilifanya upekuzi wangu na huyu Bwana anafaa. Iwapo mabunge haya yote yangejumlishwa Bw. Mwaro angepata nafasi hivi hivi. Naunga mkono uteuzi wake.

Hon. (Ms.) Mariam: Asante sana, Bw. Spika, kwa fursa hii. Kwa faida ya wanafunzi wa Kizurini naitwa mheshimiwa Mariam Mkumbi. Natoka wadi ya Kambe Ribe ambayo ni majirani zenu. Najua Kizurini ina wanafunzi wengi watokao Kambe Ribe.

Naunga mkono Mada hii asilimia mia na nina sababu mbili. Mwanzo, ni uzoefu wa kazi wa Bw. Mwaro na nilimfahamu mwaka wa 2016. Wakati huo nilikuwa mwanaharakati na zile sifa ambazo Kwale ilipewa ilikuwa nzuri, hasa katika maswala ya elimu.

Nilikuwa na kundi moja ambalo tulisafiri pamoja ili kujua ni mbinu gani huwa wanafanya hadi kuwa na sifa hizi. Bw. Mwaro ndiye aliyetupokea na kujibu maswali tuliyokuwa nayo ndipo nilipopata ufahamu kuwa huyu ni mtu wa Kilifi. Nilimuuliza waonaje ukaja Kilifi maana nimeona mnafanya kazi nzuri sana hapa? Tulikuwa tumeendea maswala mawili; moja ya elimu na *structure* ya ugatuzi. Kule kwao wakati huo walikuwa wamefika *level* ya mashinani na hilo ni jambo ambalo tulitaka kujua walifanyaje ndio kufika hapo maana sisi tulikuwa bado katika wadi.

Kulingana na yale niliyoyasoma pale, yuko na tajiriba kuu sana kuhusiana na hii nafasi ambayo ni tumpe. Pia, nimepitia hii nakala na nikaona ile Kamati ambayo imefanya hii kazi imempa asilimia 85.3 ambayo ni alama ya A. Sasa mtu akipata A, si ashapita? Sioni sababu ya mtu kupinga. Naunga mkono.

Hon. Changawa: Asante, mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii ili niongee machache juu ya mada iliyoko mbele yetu. Kwa faida ya wanafunzi, ni Mheshimiwa Emmanuel Changawa, mwakilishi wa Wadi ya Dabaso. Pia, nataka kuwajulisha wanafunzi kuwa *CV* ni Wasifu Kazi kwa Kiswahili.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Nikirudi kwa mada, nimesimama kuunga mkono Bw. Mwaro kupata nafasi hii kama Katibu wa Gatuzi la Kilifi. Nataka niseme ya kwamba kama mgeni ugenini atasifiwa mpaka apewe kiti, sasa kwao inafaa kuwa ni zaidi.

Kama Mwaro alipata nafasi hii kama Katibu wa Gatuzi la Kilifi, nataka niseme ya kwamba kama mgeni ugenini atasifiwa mpaka apewe kiti basi kwao ni zaidi. Kama Mwaro alipata nafasi hii alipoomba Gatuzi la Kwale na alipewa basi kwetu naomba kwamba waheshimiwa tumuangalie na kumpatia nafasi. Pia, napeana kongole kwa ile Kamati. Iliona vyema ya kwamba Mwaro anastahili kupata hii nafasi. Pia, kwa mara ya kwanza, mheshimiwa Spika, naona kitambulisho ambacho kiko na majina matano kwa hivyo kwa hilo nasema anafaa Martin Mwaro. Asante.

The Speaker (Hon. Mwambire): Mambo si matatu tena ni matano. Mheshimiwa Thaura Mweni.

Hon. Thaura: Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa fursa hii. Kabla nichangie Hoja ambayo iko, ningependa kuchukua nafasi hii nikaribishe wanafunzi pamoja na walimu wao. Ningependa ijulikane kwamba mmoja katika walimu ambao wamekuja na wanafunzi ni rafiki yangu wa karibu sana na pia nafikiri nitakuwa sijakosea nikimtaja hata jina, mwalimu Sanga Mdiwa ni rafiki yangu. Wacha nichukue nafasi hii nimkaribishe katika Bunge hii tukufu.

Mimi, mheshimiwa Spika, simjui moja kwa moja Bw. Mwaro. Nimekutana naye tu katika mazingira ya kazi kwa muda wa mwaka mmoja tangu tuingie katika Bunge hili. Lakini, nimemuona kwamba ni mkakamavu na ni mchapa kazi kwa hiyo sina sababu yoyote ya kumnyima nafasi hii. Kwa hiyo, mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono apate nafasi hiyo. Asante.

The Speaker (Hon. Mwambire): Mheshimiwa Grace Wambui Mwangi.

Hon. (Ms.) Grace: Asante, Bw. Spika. Kwa manufaa ya wageni, kwa majina naitwa Grace Wambui Mwangi. Sikuchaguliwa lakini niliteuliwa na chama tawala katika hii nchi, chama cha UDA *(United Democratic Alliance)*. Na nimesimama hapa kwanza nataka kushukuru Kamati ya *Appointments,* walifanya kazi nzuri kwa ile kazi waliyofanya ya kumhoji Martin Mwaro na…

The Speaker (Hon. Mwambire): Kumpiga msasa.

Hon. (Ms.) Grace: Kumpiga msasa, asante Bw. Spika. Kiswahili si chetu, tunajaribu lakini…

The Speaker (Hon. Mwambire): Si mdomo yenu, Kiswahili…

(Laughter)

Hon. (Ms.) Grace: Si mdomo chetu. Ningependa kuunga mkono uteuzi wa Bw. Martin Mwaro kwa sababu moja. Katika miaka ya nyuma, mimi binafsi na labda wengine tulitamani sana Kilifi iwe inatajwa kama Kwale. Tulitamani sana Kilifi iwe na maendeleo kama jirani yetu Kwale. Nilikuwa na maswali mengi sana vile kaunti yetu ni kubwa na ina raslimali nyingi kushinda Kwale ila ikifika ni mambo ya maendeleo ilikuwa Gavana anayetajwa Kenya nzima ni Mvurya.

Mimi binafsi nilikuwa natamani sana na nashukuru sana Kamati ya *Appointments* kwa sababu walituletea Bw. Mwaro, sababu tunajua akianza kazi… na kwa wakati mchache ambao nimemuona akifanya kazi nimekuwa nikimfuatilia sana. Kuna baadhi ya mambo ambayo tumeona akifaulu na nina uhakika huyu Bw. Martin Mwaro akipatiwa hii nafasi pia sisi tutatajika. Hata sisi miaka ijayo tutakuwa tukitajwa Kilifi ni namba moja itakuwa ni raha

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

nitajivunia. Kwa hivyo, naona tumpitishe huyu Bwana tusiangalie nyuma na naona *mood* iko sawa. Asanteni na naunga mkono.

The Speaker (Hon. Mwambire): Mheshimiwa Brown Safari.

Hon. Brown: Asante sana, Bw. Spika, kwa kunipa fursa hii mimi nami niwe mmoja katika hesabu ile ya kuunga mkono hii Hoja ya ndugu yetu na mzee wetu, Bw. Mwaro, ambaye tunamzungumzia saa hii. Kwa faida ya wanafunzi ambao wako ndani ya Bunge, jina langu naitwa mheshimiwa Brown Safari ambaye ni Mwakilishi wa Wadi ya Mtepeni. Kwa hivyo, nawakaribisha sana kwa ule mori na shauku ya kupenda kusoma ndio maana mmefika hapa pamoja na walimu wenu.

Mimi kitu cha kwanza, nitakuwa mchoyo kama sitaweza kusema hongera kwa kazi njema ambayo ilifanywa na ile Kamati. Pia, ningelipenda kupongeza juhudi zao ambazo walizifanya katika upekuzi ili kuchagua mtu ambaye anafaa kama huyu ndugu yetu, Bw. Mwaro. Tena, ningelipenda kusema kongole kwa Mwaro kupata nafasi hii maana nina amini kwamba siku ya leo tunampitisha. Nina zungumza kwa sababu tatu ama pengine zaidi kidogo nitaongezea, wasifu wake.

Wasifu wake Bw. Mwaro unafaa kupatiwa uteuzi huu wa kazi hii tukiangalia wasifu wa tajriba ya elimu, Bw. Mwaro, yuafaa katika kazi hii Kilifi hii yetu. Tukiangalia wasifu katika uteuzi wa kazi mbali mbali ambazo alihudumu katika wakati wake, Bw. Mwaro, anafaa kuwa mhudumu wetu katika Gatuzi letu la Kilifi. Tukiangalia wasifu wa utendaji kazi ambao hauna dosari ambao kila mmoja anatamani kwamba huyu bwana ni mwana wetu lakini akatumika kule Kwale sasa hivi ni wakati wetu sisi kuonyesha hisani kwamba, Bw. Mwaro, awe hapa na kutufanyia kazi barabara. Mimi naunga mkono asilimia mia kwa mia, nikiamini kwamba waheshimiwa tukiwa pamoja hapa tusipoteze wakati kumkosa mtu kama huyu. Asante na ni hayo tu.

The Speaker (Hon. Mwambire): Huwa kama uko Bungeni unasema unaunga mkono kama umemaliza husemi asanteni kama kwamba uko kwa mkutano Mheshimiwa, usiwe na hofu lakini ni Kiswahili. Usijali.

Hon. Brown: Nashukuru, Bw. Spika, bado tunaendelea kujifunza. Asante sana.

The Speaker (Hon. Mwambire): Mheshimiwa Haron Tete Ndundhi wa Mtwapa.

Hon. Tete: Asante, mheshimiwa Spika, kwa kunipa fursa hii. Moja kwa moja nasema Kiswahili kitukuzwe kwa sababu ni lugha mojawapo ambayo ndani ya Taifa letu la Kenya tunajivunia. Lugha iliyobuniwa ndani ya Taifa hili na kati ya Afrika Mashariki. Karibuni wanafunzi wa kutoka shule ya Upili ya Kizurini eneo Bunge la Kaloleni na Wadi ya eneo Kata Ndogo pia ya Kaloleni. Majina yangu ni mheshimiwa Haron Tete kutoka Shimo la Tewa. Hatuna ujirani wa sana vile lakini vile vile, Shimo la Tewa ni dunia ndogo imejaza kila aina ya kabila kutoka nchi tofauti tofauti za ulimwengu. Kwa hivyo, mpatapo nafasi, njooni masaa ya mchana.

Mheshimiwa Spika, chanda chema kivikwe pete. Mwaro anastahili kuwa kiongozi ama kuwa CS *(County Secretary)* wa Gatuzi letu la Kilifi kupitia kwa utendaji kazi wake ambao ameufanya nje ya Gatuzi la Kilifi, hasa katika Gatuzi jirani la Kwale. Ninavyoamini mimi kule uzunguni kuna wazungu weusi, ukiwasikiliza sana unaambiwa si kwao walitoka Afrika lakini walibahatika kuzaliwa kule kwa hiyo ni wazungu japo ni weusi. Martin Mwaro, tabia kwake ni Ngozi na kubadilika hataweza.

Nayasema haya kwa sababu waliosoma ni wengi na kuna wengi ambao labda walisoma zaidi yake lakini utendaji kazi wake umethibithisha ya kwamba kwake ni tabia ya kutaka kutenda kazi kwa usawa, kuweka ahadi zake kwa ajili ya kwamba hata kwetu awe taa ama nuru na kielelezo hata kwa jamii nyengine ama kwa vizazi vingine vijavyo. Kwa sababu yeye ni

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

kielelezo, jina hujengwa na matendo; Mwaro yuatajika kwa sababu ya matendo yake, ni wengi ambao tuna majina mazuri yenye ufupi wa herufi, ufupi wa kufanana na sisi wenyewe lakini hatuna umbali tulio sikika kwa sababu maneno yetu na utendaji kazi wetu, haujafanana na masomo yetu.

Huyu bwana nasimama nikisema ninamuunga mkono vilivyo; si kwa sababu ya aina yeyote ambayo ina msukumo ila utendaji kazi wake umenipea nafasi ya kutamani ndani ya Kilifi Kaunti ama gatuzi letu hili tuwe na mtu ambaye atakuwa anatetea jamii kwa kutenda kazi sawa sawa. Huyu bwana siwezi kumtukuza lakini hata wale maadui, kuna wimbo unasema ombea adui yako aishi siku nyingi ili baraka zako zikifika azishuhudie kwa macho. Wale ambao hawamtakii mema bwana Mwaro, nawaombea waishi siku nyingi ili siku zake za kubarikiwa wazione, baraka zake zikiwa zitawasaidia hata hao wenyewe. Asante na naunga mkono.

The Speaker (Hon. Mwambire): Maybe for the benefit of others; not just Africans who are black even Caribbeans and when I visited India, I saw even some Indians are black. So, do not assume that only Africans are back.

The Leader of Minority (Hon. Mumba): Nichukue fursa hii, mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru Mwenyezi Mungu kwa hii fursa ambayo ametupatia sote kuweza kuwepo katika Bunge hii. Vile vile, pia nichukue fursa hii nishukuru kwa kuweza kunitunuku hii nafasi ili niweze kupeana changizo zangu katika Hoja ambayo ipo mbele ya Bunge hili.

Niruhusu kwanza niende nje ya Bunge hili, kisha nitarudi hapa nikimaliza changizo hizi. Mengi yamenenwa na mengi yamezungumzwa na yote yanaelekeza katika wema na uzuri na vile vile kwa manufaa ya Gatuzi hili letu la Kilifi.

Kwanza, nataka nichukue fursa ya kipekee niweze kumpongeza mstahiki Gavana kwa kuweza kuchukua hatua ya kwanza kuleta lile jopo ambalo lilihusika katika kuwachunguza na kuweza kuthibithisha kwamba jina hili ambalo tunalizungumzia leo akiwa kwamba ndio mteule wa Katibu wa kata ama jimbo na vile vile Mkuu wa Utumishi wa umma katika Gatuzi letu la Kilifi.

Lile jopo lilifanya kazi nzuri na ndio maana leo sifa zote zimeweza kumiminika hapa kuhusiana na bwana Mwaro. Kwa hivyo, hiyo ni kazi ambayo ilianzia mbali… naambiwa kuna dhana mheshimiwa Spika… asante kwa hivyo nimeona ni vyema niweze kutambua weledi wake na ukakamavu wake ndio maana akatupatia bwana huyu ambaye amehitimu.

Nikirudi katika Bunge letu, mheshimiwa Spika, nashukuru Mwenye Mungu amenipatia macho mazuri ya kuona nataka nichukue fursa hii ya kipekee kwanza nikupongeze mheshimiwa Spika, pamoja na Katibu wa Bunge hili. Maana nilipoingia hapa ndani kila mmoja namwona kwa sura ikiwa anaonekana, siku za nyumani mwangaza wetu ulikuwa mchache hapa ndani lakini leo hata sindano ikianguka nitaiona kwa sababu mwangaza ni mwingi na ni mzuri. Hii ni ishara ya kazi nzuri ambayo inaendelea hapa Bunge ili kutuwekea mazingira mazuri ya kuweza kutekeleza wajibu ambao tumeweza kuitwa tuufanye tunapokuwa hapa.

Pongezi pia kwa hiyo kazi nzuri; najua wengine wananga'ariwa na hawajui tofauti iko wapi. Kumbe kuna mambo mazuri yamefanyika hapa. Vile vile, pia nilipoingia hapa nimeona vibandiko vya kutambua viongozi wa Bunge, pale nyuma ilikuwa aibu sana. Unakuta ni karatasi limebadikwa kwenye kiti, mara limebambuka, lakini leo hii nilipoona ishara ya vibandiko katika meza zetu nikaona kwamba ni hatua kubwa ambayo tumeweza kuipiga. Kwa hivyo, nitakapokosa kuwashukuru na kuwapongeza vile vile, nitakuwa naona siitendei haki ule mwelekeo ambao mmeuchukua. Kwa hivyo, pongezi.

Mimi, yangu ni machache kwa sababu ni ada tu kwamba niweze kuzungumza lakini ishara na ni bayana kwamba sote tumeridhia kwamba Bw. Martin Mwaro alivyoteuliwa katika

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

nafasi hii, tajiriba yake, ujuzi wake, uzoefu wake wa kazi na ukiangalia pia wasifu wake wa kazi, kwa kweli hatuna pingamizi ya bwana Mwaro kuweza kuchukua nafasi hii.

Na ikumbukwe kwamba, ameweza kuikaimu kazi hii kwa muda wa mwaka mzima na tumeona tayari utendajikazi wake. Ukiangalia upande wa elimu na upande wa masomo, huyu bwana katika upekuzi wangu, katika ile Kamati niliona kwamba amejizatiti, amejikakamua, amebukua vitabu na amefikia hadi shahada ya uzamili.

Na katika udadisi wangu alinitaarifu kwamba ile ya uzamifu pia nayo anainyemelea na huenda karibuni akaweza kuipata. Kwa hivyo, ni mtu ambaye ana ari ya kuweza kujiwekea elimu na kuweza kutafuta kujua zaidi. Kwa hivyo, katika uzoefu na katika elimu ambayo yuko nayo, nina imani kwamba tuko mahali pa sawa na atatekeleza wajibu wake kwa njia ya sawa na tunatarajia manufaa katika nafasi ile atakavyoendesha pamoja na mstahiki Gavana wa gatuzi letu la Kilifi. Kwa mukhtasari, mheshimiwa Spika, nasema naunga mkono na mimi kama kiongozi wa Wachache ninapounga mkono huwa hii Hoja ishapita. Asante.

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Asante, Bwana Spika, kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza, ningeomba nijitambulishe ili wanafuzi wanielewe. Kwa majina naitwa Ibrahim Abdi Athman, mimi ni MCA (*Member of County Assembly*) wa Wadi ya eneo Bunge la *Kilifi North*. Mimi ndiye Kiongozi wa Wengi katika Bunge hili. Mkiangalia hapa mtaona *Majority Leader*. Kule kwenu nyinyi wanafunzi mko na kiranja, na sisi hapa tuko na *Majority*. Sasa, hawa waheshimiwa wote, ile mipangilio yao yote ni lazima ipitie kwangu ndio maana mnaona hata nywele nyeupe zimeanza kunitoka kwa sababu napambana na kazi ngumu.

Pili, kuweni watulivu, karibuni sana wanafunzi wa Kizurini. Hili ni Bunge la Tatu katika historia yetu ya Jimbo letu la Kilifi. Tuko na waheshimiwa hamsini na moja (51) katika Bunge hili; thelathini na tano (35) ni wale ambao wamechaguliwa na wananchi na kumi na sita (16) ni wale wameletwa hapa na vyama. Bunge hili, tuko na vyama tofauti tofauti; tuko na chama cha PAA (*Pamoja African Alliance*), UDA (*United Democratic Alliance*) na tuko na vyama vya ODM (*Orange Democratic Movement*). Wale ambao wako wengi hapa ni wa chama cha ODM na pia kuna *Independent*.

Bw. Spika, kuna umuhimu kwa sababu mimi kama Kiongozi wa Walio Wengi kwa Bunge hili, nataka kuwapatia mafunzo kidogo wanafunzi hawa. Wanafunzi karibuni sana. Mheshimiwa wenu ambaye ni Birya Fondo ni mheshimiwa mkakamavu; ni mheshimiwa mchapakazi ndani ya Bunge hili. Ni mtu ambaye huwa analeta Miswada mingi sana. Nataka pia mkifika nyumbani muwapongeze wazazi wenu kwa kumchagua mheshimiwa Birya Fondo kwa sababu ni mchapa kazi.

Wanafunzi, mkijisikia kwenda haja hakuna shida. Hatungependa mchafuane hewa hapo, msiwe waoga. Askari hawa watawaelekeza katika Bunge hili. Wanafunzi najua mnaenda kufanya mtihani na mtihani usiwatishe. Kufanya mtihani, upite ama usipite sio mwisho wa maisha. Nataka niwaambie mtie bidi. Sisi tunawaombea Mungu muwe na matokeo bora. Mnajuana nyinyi na mimi najua ya kwamba katika masomo yenu sisi kama waheshimiwa tunakaa hapa kwa kipindi cha miaka mitano na mtihani wetu unakuja baada ya miaka mitano. Nyinyi mtihani wenu unakuja baada ya miaka minne. Najua kuna wale watapata na kuna wale watakosa; sio kwamba ukifeli katika mtihani ndio mwisho wa maisha. Fanyeni bidii mpambane na maisha. Hata sisi hapa hivi mnavyotuona tumeshajuana ni nani ambaye atarudi na ni nani ambaye hatarudi.

(Laughter)

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Ndio maana mnaona ya kwamba, hii kazi ambayo iko hapa sio kazi rahisi; ni kazi ngumu. Hapa hamuoni mzungu wala mhindi; sote ni wamijikenda na sote ni Wanakilifi ndio maana mumeona hata wengine Kiswahili kinawatatiza. Wanapewa nafasi na Spika lakini Kiswahili kinawatatiza na wakitoka huko nje utawaona wao ndio na parapara nyingi sana. Hayo ni maisha wanafunzi wangu.

(Laughter)

Mmekuja siku nzuri leo kwani tuko na Miswada mingi sana ya kupitisha. Karibuni katika Bunge hili na nawatakia kila la heri na Mungu awabariki. Kwa kuongezea, niwapatie mfano kidogo ya kwamba nimerudi nikawaambia kukosa masomo sio mwisho wa maisha. Hapa ndani ya Bunge hili tuko na madaktari wamekosa wateja ndani ya zahanati, walifungua zahanati lakini wateja wakakataa ndio wakajaribu uheshimiwa na ndio maana wako hapa. Kwa hivyo, tuko na madaktari, tuko na ma *Engineer*, na tuko wa walimu hapa ambao pia wao walifungua shule hawakupata wanafunzi lakini wako hapa. Kwa hivyo, wanafunzi msijali na mimi nina uhakika baadhi yenu watafika hapa. Karibuni.

(Applause)

Bw. Spika, nataka kusema kwamba naunga mkono Bw. Mwaro awe *County Secretary* wa Jimbo letu la Kilifi na utendakazi wake tumeuona. Kwa hivyo, Bw. Spika, sitaki kuongea mambo mengi kwa sababu yameongelewa na waheshimiwa na pia kuna kazi nyengine ambazo zinatusubiri. Kwa hayo machache, asanteni na Mungu awabariki.

(Question, that the Mover be now called upon to reply, put and agreed to)

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Asante, Bw. Spika. Kwanza, napokea pongezi ambazo zimetoka kwa waheshimiwa walipokuwa wakichangia Hoja hii na pia kwa imani ambayo Bunge hili limekuwa na Kamati ambayo Mwenyekiti wake ni wewe, Bw. Spika.

Pia, ningetaka kumpongeza Gavana wetu kwa kuangalia kile ambacho kilikuwa ni bora katika ile orodha ambayo alipokea ya wale waliotahiniwa kwa nafasi hii ambayo jina moja liliweza kutufikia hapa. Mwisho, kumpa pongezi mwanakilifi kwa vile alivyotuletea katika Bunge hili waheshimiwa ambao wana maono ya kuuleta uongozi ambao ni wa kufaidisha jimbo letu la Kilifi.

Kwa hivyo, zangu ni shukrani kwa ushirikiano ambao tumekuwa nao haswa katika kupitisha Hoja hii ya kumuweka Bw. Martin Mwaro kuwa *County Secretary* wa jimbo hili la Kilifi. Asanteni.

(Question put and agreed to)

ADOPTION OF THE REPORT ON THE VETTING OF NOMINEES TO POSITIONS OF CHAIRPERSON AND MEMBERS OF THE COUNTY PUBLIC SERVICE BOARD

Hon. Zia: Asante, mheshimiwa Spika. Ripoti ilitayarishwa kwa Kiingereza lakini nitaiongelea kwa Kiswahili ili wanafunzi waweze kujuzika. Ningependa kuendesha mjadala kwa Bunge hii ili waweze kuikubali Ripoti ya Kamati ya Ugatuzi, Utumishi wa Umma na Majanga

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

iliyokagua na kupiga msasa Mwenyekiti na watatu walioteuliwa kwa nyadhifa kwenye Bodi ya Uajiri katika Gatuzi letu la Kilifi ambayo imeweza kuwekwa kwa Bunge hivi leo Jumatano ya tarehe sita mwezi wa Tisa mwaka wa 2023.

Kabla sijaita atakayeunga mkono hii Ripoti, sisi katika Kamati ya Gatuzi, Utumishi wa Umma na Majanga watu ambao waliweza kuletwa ni wanne lakini tuliweza kukagua watu watatu ambao ni Mwenyekiti ambaye anaitwa Albert Joseph Mturi akiwa ni Mwenyekiti katika hiyo Bodi. Wa pili, ni Attas Shariff Ali na wa tatu alikuwa ni Susan Kadzo Mumba. Yule wa nne ambaye hakuweza kufika katika Kamati yetu anaitwa Francis Fondo.

Mheshimiwa Spika, kulingana na ukaguzi wetu, watatu wale tuliwapitisha kama Kamati na tukakubaliana kwamba Bw. Albert Joseph Mturi awe Mwenyekiti. Tulipitisha wa pili, Attas Shariff Ali kuwa mwanabodi na watatu Susan Kadzo Mumba kuwa mwanabodi pia wa bodi ya Utumishi wa Umma. Kulingana na ukaguzi wetu, hawa watu hawakuweza kushitakiwa katika korti yoyote ndani ya Kenya. Nikisema hivyo hakuna kesi yoyote kuanzia kwa mzee wa kijiji hadi juu. Katika tajriba, tuliwapata wako na wasifu kazi nzuri. Naomba waheshimiwa wapitie vizuri ili…

The Speaker (Hon. Mwambire)**:** Kiongozi wa Wengi ako na Hoja angependa kuiweka Bungeni.

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Asante, Bw. Spika. Mnenaji anasema kwamba alihakikisha kuwa hawajashtakiwa kwa Chifu, kwa wazee wa vijiji...Je, Mwenyekiti anayo stakabadhi yoyote ya kuonyesha anayonena ni ya ukweli? Kuna umuhimu wa kujua kama stakabadhi hizo ziko kwenye Ripoti hii. Huwa kuna *Certificate of Good Conduct* kutoka DCI *(Directorate of Criminal Investigations*) lakini sijaona kuwa kuna *certificate* kutoka kwa *Chief's office* na amehakikisha kama Mwenyekiti, je jambo hili linajitokeza kama la mzaha ama Mwenyekiti hajui analosema?

The Speaker (Hon. Mwambire): Pia, mheshimiwa kwa sababu wewe ni mjuaji wa Kiswahili, ungemrekebisha kuhusu lile neno bodi; sijui kama ametohoa lakini neno sahihi ni Halmashauri.

Hon. Zia: Asante, Bw. Spika. Kiongozi wa Wengi kama ulivyosema ni mkwasi wa Kiswahili lakini la sivyo. Nataka kurekebisha kwamba kitu chochote ambacho kinatoka upande wa Idara ya Ujasusi (DCI), wale wako na ripoti nyingi kwa hiyo chochote utakachokifanya hata ikiwa mashinani wao pia hupata Habari. Wacha tuwachie hapo ili tusaidie wakati. Hawa tuliwakagua na tukapata kuwa hawana dosari; wako safi na weledi wa kazi. Naomba wenzangu waungane nami ili kuwapitisha hawa na tufanye kazi kwa umakini.

Kabla sijakaa, nataka nimuite atakayeunga mkono Ripoti hii Mheshimiwa Mariam Mukumbi ili aweze kuunga mkono.

The Speaker (Hon. Mwambire)**:** Mwalimu Sanga Mdiwa kutoka ile shule iliyotutembelea atatupa alama ya wale watakaokuwa wamenena Kiswahili bora zaidi maana nimefahamishwa kuwa yuko hapa.

Hon. (Ms.) Mariam: Asante sana, Bw. Spika. Nasimama kuunga mkono Ripoti hii ya uteuzi wa Bw. Albert Mturi kama Mweyekiti na Attas na Susan kama wanakamati wale watatu tuliowafanyia ukaguzi. Kama vile Mwenyekiti alivyosema, sitaki kuchukua muda mrefu kwa sababu kama mmoja wa wanakamati nilikuwa pale katika kupiga msasa hawa watu na kulingana na yale mahojiano na majibu tuliyopata tuliona hawa watu wanastahili na pia ukiangalia kielimu, ni watu walio na tajiriba na uwezo wa kufanya hii kazi. Naunga mkono.

(Question proposed)

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. (Ms.) Radhia: Asante sana, Bw. Spika, kwa nafasi hii. Nimeomba nafasi hii kwa muda mrefu sijui kama mashini yangu ni mbaya ama hukuvaa miwani. Nashukuru pia kwa kuwa walipitishwa katika Kamati na nimesimama kuunga mkono Ripoti iliyo mbele yetu ya hawa watu watatu.

Kwanza kabisa, nashukuru Mungu kwa kufika kwa wanafunzi kutoka jimbo letu kuja kuona tunachofanya katika Bunge. Nataka kuwajulisha wanafunzi, kila aliyesimama hapa leo anaongea Kiswahili, mkitoka hapa mjue pia tuko na wazungumzaji wa Kizungu hata wengine wakiongea mtashindwa hata kutafsiri. Watu leo wako na *mood* nzuri na wakiwa hivyo, hutaka kuongea kikwao ili afahamike zaidi; hata wale ambao hawakusoma waelewe zaidi na ki urahisi wasitafute mkalimani aweze kuwatafsiria yalioongewa ndio nikaona waheshimiwa wote hapa leo kila anayeinuka anaongea Kiswahili. Sio kwamba hilo Bunge halina wasemaji wa Kizungu. Tuna madaktari kama mlivyoambiwa, tuna ma *engineer* hapa, tuna walimu na vipawa vingine vya kikazi. Kwa hivyo, nataka ifahamike mkitoka hapa msiseme tumekwenda Bungeni na tumepata watu wote wazungumza Kiswahili. Ni vipi? Ni hivyo, hivyo nilivyowafahamisha.

Katika hawa watu watatu, sisi hapa Bungeni tuna Kamati zetu za kila… sijui nitaiongelea vipi. Kila Idara ina Kamati na hiyo Kamati ni waheshimiwa wa Bunge hili ambao ni watu wenye ukakamavu wa kuweza kukagua nani anafaa na nani hafai.

Kwa hivyo, kama mheshimiwa Radhia ninapofika hapa ikiwa Ripoti imeletwa na wenzangu huwa mara nyingi sipendi kuipinga kwa sababu najua waliokwenda pale walikuwa na makini ya kufanya kazi zao. Katika hawa watatu, nitasema huyu Attas Sharif nimemjua kwa miaka mingi. Najua fika mheshimiwa Spika hii nafasi akiwa ataweza kuipata basi atafanya mabadiliko ndani ya hii Kilifi kwa sababu nitasema kama hii ni Idara yake.

Amefanya kazi pale Mida; amehudumia wananchi wa Malindi na Kilifi nzima na tumeona utendakazi wake pale alipokuwa akisaidia Kamati. Kwa hiyo, nina imani kubwa atakapofika pale atatoa mchango mkubwa kwa yale aliyokuwa akifanya kule mwanzo. Na mama Susan pia naye, na Mturi, nina hakika watakwenda kututendea kazi inayofaa na itawanufaisha wananchi wote wa Kilifi. Nawaombea kila la kheri na wasiwe na ubaguzi wa dini wala ya rangi wala ya kabila. Naomba waende pale na nguvu zote na wafanye kila ambalo linalazimu kufanywa.

Nikimalizia, nimesimama kuunga mkono na majina yangu kamili wanafunzi naitwa Radhai Ali Omar. Mimi ni mheshimiwa wa kuteuliwa kipindi cha pili. Kwa hivyo, yote yawezekana wanangu, bidii kwa nguvu na mfanye bidii mpite japo Kiongozi wa Walio Wengi amewambia kuanguka kwa mtihani sio mwisho wa maisha, ndio lakini mfanye bidii mpite. Kwa sababu, ukitoka na D ama C- huna mahali utaenda ni lazima wewe mwenyewe kama mwanafunzi pia utakufa moyo mapema na utaona ndio mwisho wa maisha.

Ndio, sio mwisho wa maisha, lakini kama Mwaro alituletea ma *certificate* mengi itakuwa vigumu wanangu? Kwa hivyo, ni mfanye bidii msome mpite kesho mkija hapa tena tuwapate munaleta makaratasi yenu kama hawa walioleta ya kwamba tayari wana stakabadhi za kutosha. Mbali na kujuana, kuna stakabadhi za kutosha mpaka ulete ndio upite. Kwa hayo machache, nimesimama kuunga mkono.

The Speaker (Hon. Mwambire): Mheshimiwa Anzazi Maneno.

Hon. (Ms.) Maneno: Asante sana, Bw. Spika, kwa kunipatia nafasi hii. Pia, nimesimama kuungana na wenzangu ili niweze kuunga mkono Ripoti hii ya Kamati ya Ugatuzi. Ninawapatia kongole wanakamati, ninampatia kongole Bw. Gavana; nikiangalia haya majina nimeona Bw. Albert Joseph Mturi, ambaye tukipitisha siku ya leo atakuwa yeye ndiye Mwenyekiti wa hii

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Bodi. Nataka kujuza Bunge hili kwamba Albert anatoka kwa wale ambao ni wakaazi wa Kilifi wachache. Bw. Albert anatoka Kambe Ribe; tukiangalia hizo ni kabila mbili zimechanganywa zikaweza kuleta wadi moja. Kwa hivyo wengi walikuwa… nimekuwa kile kipindi chengine na hiyo miaka mengine ya nyuma ya ugatuzi…

The Speaker (Hon. Mwambire): Mheshimiwa, historia inakwambia kwamba walio wachache ni Wa Pemba hapa katika Gatuzi la Kilifi.

Hon. (Ms.) Maneno: Wa Kambe, Wa Ribe, Wa Pemba wote ni wachache tukilinganisha na kabila lengine la Mchonyi na Mgiriama. Mijikenda *in general*…

The Speaker (Hon. Mwambire): Sasa umechanganya wanafunzi, *general* ni?

Hon. (Ms.) Maneno: Spika, tafadhali naomba nimalize, nipe nafasi nimalize.

The Speaker (Hon. Mwambire): Najua umeambiwa ni mwalimu na mimi sijajua ndio nataka kupata ufahamu kidogo.

Hon. (Ms.) Maneno: Kwa jumla.

The Speaker (Hon. Mwambire): Oh sawa, endelea mwalimu.

Hon. (Ms.) Maneno: Asante, Bw. Spika. Kwa hivyo ni kongole. Tukiangalia Kenya nzima hakuna mahali ambapo wale ambao ni wachache wamepewa kiti kama hichi. Kwa hivyo Bw. Albert, Bw. Sharif na Mama Susan, ombi langu kwao ni wafanye kazi kwa uaminifu na kwa uwazi, maana Kaunti ya Kilifi yote inawaangalia wao jinsi wataendesha mambo hasa yale ambayo huwa yanaleta utata wa kazi. Mheshimiwa ambaye amenitangulia, mheshimiwa Radhia amesema kusiwe na ubaguzi wa kabila au wa dini na mambo mengine; wahakikishe wanafanya kazi vizuri na wanarudisha hadhi ya Kilifi mahali ilipokuwa. Kwa hayo machache, asante na ninabaki kuunga mkono Ripoti hii.

The Speaker (Hon. Mwambire): Mheshimiwa Koki.

Hon. (Ms.) Koki: Asante, Bw. Spika, kwa kunipatia nafasi hii ili pia niweze kuunga mkono Ripoti hii. Nataka kuwapongeza wanakamati, nikiwa mmoja katika wanakamati waliokaa na kuandika Ripoti hii na pia kupongeza *Secretariat* iliyotufanyia hii kazi na tukaweza kuleta haya majina matatu hapa Bungeni likiwa la kwanza ni la Bw. Albert Mturi, Attas Ali na mama Susan Mumba. Kwa niaba ya wakaazi wa Mariakani ambao walinileta katika Bunge hili, nasimama kuunga mkono Ripoti hii kwa sababu sasa hivi nitakaporudi Mariakani nitaweza kuwaambia wale vijana, kina mama na watu wanaoishi na ulemavu kuwa mambo karibuni yatakuwa mazuri hata kama ni ajira mbili tatu katika vijana wetu wataenda kupata hizi nafasi.

Pili, nataka kusema kuwa tutakapoenda kupitisha halmashauri hii basi tuweza kusaidia mkaazi wa Kilifi ili ile kazi ya Kilifi iende kutimia. Tatu, ni kuwa watu hawa wataweza kwenda kutimiza majukumu yao kulingana na sheria. Mimi nikiwa nimetoka kule Mariakani, kunao vijana wangu wengi sana walikuwa wamechukuliwa kama vibarua; pengine sasa wataweza kubahatika na kuweza kuandikwa na kuweza kupata mishahara maana hata mishahara wamekuwa hawapati. Kwa hivyo, naunga mia kwa mia na wakati umeenda na sidhani kama kuna yoyote hapa ataenda kupinga kwa hivyo uliza swali tu tusonge mbele.

The Speaker (Hon. Mwambire): Mheshimiwa Shehe.

Hon. Shehe: Asante sana msemaji wa Bunge letu la Ugatuzi la Kilifi kwa kuwafahamisha wageni wetu waliko hapa jina langu naitwa mheshimiwa Peter Safari Shehe, nikiwa natoka Jaribuni ambaye ni MCA (*Member of County Assembly*) wa kwanza Kenya nzima alikuwa Mbunge. Lakini niko hapa kufanya kazi na wenzangu ambao tuko hapa kupata elimu ya kufundishana, kutunga sheria na kusukuma hili dau ambalo ni la Kilifi. Sasa tukiwa tuko hapa, nataka kuwafahamisha wanafunzi wa Kizurini mlivyosikia jina langu mimi ni mwanafunzi wa Kizurini miaka ya zamani.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

(Applause)

Ndiposa nafikiria msemaji wa Bunge letu ameona afadhali nisimame niwasalimie. mkifika huko, kuna Peter Safari Shehe, alikuwa akisoma Kizurini. Wakati huo bado ilikuwa *Primary* ilikuwa haijakuwa *Secondary*. Hata hivyo, ninapenda kuipongeza Kamati ya Ugatuzi iliyofanya hii kazi kubwa sana ya kupambana na mchujo waliokuwa nao wa kutafuta wale watu ambao wanaweza kustahamili hii hali ambayo tumekuwa nayo ya utata mwingi sana tunapoingia kazi.

Nina swali moja; yule wa tatu ama yule mwingine ambaye hakuja labda pengine tungepata kujua ilikuwa vipi mpaka ikawa hakuja? Aliambiwa asije, ama alikataa? Jibu hilo pengine mnaweza kujua na ni kwa sababu gani… alikuwa pengine ana shida fulani ambayo ilimfanya asije bila kutoa salamu zozote.

Hata hivyo, waliochaguliwa tuwape kongole na wawe watahudumia wana Kilifi ambapo tumekuwa na utata mwingi sana wa uandikaji wa wafanyikazi. Watu wamepata shida, unaweza kukuta watu wamekuwa katika utendaji kazi miaka kumi (10) bila kupata karatasi ama thibithisho la kusema ama la kujulikana wanafanya kazi Kilifi Kaunti; ni kibarua tu ama *volunteering* ama mambo mengine yasiyo na msingi. Halafu, ukisikiza hata Ripoti ama kuandika, kueleza kazi wanayofanya hao watu walikuwa hawajui.

Bajeti zote walizokuwa nazo, lakini walikuwa hawawezi kuandika. Ni kitu cha kusikitisha sana, natarajia kwamba safari hii waliopatikana watatusaidia sisi watu wa Kilifi na nyinyi mkienda nyumbani mkifika huko mjue kwamba Spika wetu na wafanyaji kazi wa Kaunti ya Kilifi na waheshimiwa wote wanashirikiana vilivyo kutoa hali ambayo itakuwa ni hali ya juu ya Kilifi. Hatutaki Kilifi yetu iende chini, ila tunataka kuienua ndiposa kuna hali ambayo mmeambiwa kuna madaktari hapa, kuna ma *architects* hapa na watu wa tajriba tofauti tofauti. Spika mwenyewe amekuwa katika Bunge la Kitaifa na yuko hapa, kwa hivyo kuna uhakika ya kwamba kazi itatendeka. Naunga mkono moja kwa moja, mheshimiwa Spika, tukiwa tuko katika njia ya kisawasawa. Asante.

Hon. (Ms.) Lilian: Asante sana, Bw. Spika, kwa kunipatia nafasi hii mimi pia niweze kuchangia machache na pia ningeweza kuunga mkono Kamati husika iliyofanya kazi nikiwa mwenyekiti mdogo. Kusema ile ukweli, tuliweza kufanya kazi iwezekanavyo.

Kwanza, tuliweza kuwahoji wahusika, neno moja kwa moja na waliweza kujibu maswali. Hata mengine kabla hujamuuliza anajibu kumaanisha ni watenda kazi vilivyo. Ukimwangalia Mturi, aliweza kujieleza vizuri na tukampatia mia kwa mia.

Susan pia naye aliweza kujieleza vizuri, tukamuuliza maswali akajibu iwezekanavyo tukampatia mia kwa mia. Atthas naye pia, tuliweza kumuuliza na pia anajua maeneo Bunge mengi. Alitutajia Mariakani anakujua mpaka Chasimba na kila mahali na tukawa na furaha kuu ya ajabu. Kukitoka kijana Chasimba akija akimwelezea atajua anatoka wapi na ni eneo Bunge liko aina gani.

Tulishukuru na pia naunga mkono vilivyo na pia waheshimiwa wenzetu tungeomba tuweze kuunga mkono ili hawa waweze kufanya kazi na Kilifi yetu iweze kusonga mbele. Asante naunga mkono mia kwa mia.

Hon. Thaura: Mheshimiwa Spika, nasimama kwa Hoja ya nidhamu nambari tisaini na mbili (92). Ukiangalia taswira ya Bunge kwa namna ilivyo sasa na hisia za hii Bunge nadhani kwamba waheshimiwa tunaendelea kujirudia japo kwa mazuri. Lakini ninaomba kwa unyenyekevu kwamba ikiwezekana kupitia Hoja hiyo ya nidhamu namba 92 kwamba uulize

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

swali tu, mheshimiwa Spika, ili kwa kauli moja nafikiri unavyoiona Bunge ni kwamba sisi sote tuna mtazamo mmoja, ili tupate nafasi ya kufanya shughuli nyingine. Ninakuomba kwa unyenyekevu.

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Members, in reaction to the Standing Order that has been cited it requires me to put the question so that I can ascertain that that is the position. So, I will put the question so that I can confirm whether the mood of the House is that, or I call the Mover to respond, or we proceed with the debate.

(Question, that the Mover be now called upon to reply, put and agreed to)

Hon. Zia: Asante sana, mheshimiwa Spika. Kwanza, wacha nishukuru waheshimiwa wenzangu kwa kuweza kuchangia mjadala ambao nimeweza kuleta kwa niaba ya Kamati yetu ya Gatuzi. Nakushukuru pia, Bw. Spika, kwa mwelekeo ama mwelekezo ambao umekuwa nao ndani ya hili Bunge. Kwa hivyo, Mungu awabariki ndugu zanguni ambao mko hapa. Asanteni sana.

(Question put and agreed to)

ADOPTION OF THE REPORT ON THE VETTING OF NOMINEES TO THE MALINDI MUNICIPALITY BOARD

Hon. Ray: Thank you, Mr. Speaker, Sir. I beg to move the following Motion: -

THAT, this House adopts the Report of the Lands, Physical Planning and Urban Development Committee on the Vetting of nominees to the positions of Members of the Board for Malindi Municipality laid on the Table of this House on Wednesday, 6th September 2023.

Before I ask my fellow Member to second this Motion, I have my submissions. In my submissions I would like to first thank my fellow Committee Members, the secretariat and on behalf of my Committee Members, I would like to thank your Office and also the Office of the Clerk for all the necessary arrangements during this time of vetting. I would also like to inform the House that the County Assembly of Kilifi received from the Office of the County Secretary the nomination of the Malindi Municipality Board for the position of Board Members in charge of the Municipality. The said nominations were committed to the Sectoral Committee on Lands, Physical Planning and Urban Development during the plenary sitting of Friday, 11th August 2023 for vetting and thereafter making a Report to the County Assembly. I would like to mention the names of the nominees as: -

1. Amir Mansour Naji
2. Conrad Angaga Atiang
3. Balal Abdulaziz Chaudhri
4. Suileman Salim Omar
5. Clara Mukhambe Muganga
6. Alice Mwaka Matembo
7. Agness M. Mturi

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

As the Committee, the nominees who appeared before us were six but the seventh one, Balal Abdulaziz Chaudhri did not make it on this date. I am informed that he communicated to the Clerk, and I think there are arrangements, a date to be set later for him to appear before us.

The members of the public were given an opportunity to be in this vetting session and they were also asked if they had any memorandum or petition they could take to the Clerk of the County Assembly after which, Mr. Speaker, the nominees were vetted in accordance with the Public Appointments (County Assemblies Approval) Act, 2017, the Urban Areas and Cities Act, 2011 and the County Assembly Standing Orders using the following criteria amongst others. That is academic qualification, employment record, professional affiliation, potential conflict of interest, knowledge of the relevant subject, overall suitability for the position, tax compliance and integrity.

After going through this vetting process for all the nominees, we made some observations and findings, and one is that the Board was properly composed in terms of the constitution. The issues of youth and gender were catered for, and the nominees had never been adversely mentioned in any investigatory report of the County Assembly or any other commission of inquiry in the last three years.

The nominees also had requisite qualifications and experience in the public service which qualifies them to the position of Board Member of the Malindi Municipality.

The nominees also articulated topical issues in the line of the Department and showed professionalism and technical capabilities. All the six nominees we vetted got marks suitable for them to fit in this position on the Board and after all the findings the Committee also recommended the following at the end of the vetting process;

Having considered the suitability, capacity, and integrity of the nominee and pursuant to Section 45 of the County Governments Act, 2012, County Assembly Standing Orders 43(4) and the Public Appointments (County Assemblies Approval) Act, 2017, the Committee recommends that the County Assembly of Kilifi approves the nominations and the subsequent appointments of all the nominees as Board members of the Malindi Municipality. Thank you.

The Speaker (Hon. Mwambire): Is it for all those who appeared?

Hon. Ray: For the six nominees, yes.

The Speaker (Hon. Mwambire): Thank you. Who is seconding?

Hon. Ray: May I ask hon. Tete to second.

Hon. Tete: Asante, Bw. Spika, kwa nafasi hii. Napenda kuunga mkono kazi ya Kamati. Nitaanza kusema kwamba chura kuishi ndani ya maji ni starehe na sio usafi. Nayazungumza haya kwa sababu mazungumzo mengi yaliyotangulia hapo nyuma kuna mheshimiwa amesema ya kwamba kunao wenye kusihi katika kabila ndogo ndogo ndani ya Kenya na kabila hizi ndogo zisiwe sababu za hao kwamba watambulike kikazi pasipokuwa na utendaji. Nikisema hivyo, mimi nikiwa katika kabila kubwa la Ugiriama haimaanishi kuwa ni *opportunity* ya mimi kuajiriwa na niwapo katika kabila ndogo nipate huruma za kuenda kuharibu mahali. Nataka niseme kwamba utendajikazi wako na jinsi utakavyojizatiti na utekelezaji wako wa Kamati utakavyoangaliwa kila utakachokipewa kinakustahili.

Kwa hivyo, wale wote ambao wamepitia mitihani hii ambayo wamefika katika Kamati kuangaliwa na kuonekana kwamba wanafaa, tusiangalie katika mirengo ya kabila wala dini wala ujirani. Kaunti ya Kilifi inataka kutendewa kazi na watu wenye hadhi na heshima na watetezi watakaoangalia kizazi kijacho kwamba kitakuwa wapi kupitia kwa uteuzi huu ambao tunauweka leo. Iwapo kuna mahali tutaharibu, lawama haitaelekea mahali pengine lakini katika Bunge hili tulilosimama leo.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Nataka kusema ya kwamba wote ambao wamepitia katika kuhoji nawaunga mkono kwa sababu ni wakenya na wameangaliwa wanastahili, sina sababu za kupinga na kwa sababu hiyo ninaafiki. Asante.

(Question proposed)

Hon. Oscar: Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa fursa hii. Naona kuweka changizo katika Hoja ile ya kwanza haikuwa rahisi lakini nashukuru kwa nafasi hii. Kwa niaba ya wale wageni, kwa jina naitwa Oscar Wanje, Mwakilishi Wadi wa Ganda. Mimi ndio Mwakilishi aliyeteuliwa na kura ambaye ndiye mdogo kabisa hapa Bungeni. Kwa hivyo, karibuni sana, Kizurini …

The Speaker (Hon. Mwambire): Ni mdogo kimwili, kiumri ama…

Hon. Oscar: Ni mdogo kiumri. Shule ya Kizurini naifahamu vizuri kwa sababu mimi nimesoma Ribe *Boys High School*; nimemaliza mwaka wa 2011. Nyinyi mlikuwa washindani wetu kwa hivyo, karibuni sana na nawatakia kila la kheri wakati mkifanya mtihani wenu na mfuzu vizuri kama jina lenu la shule Kizurini. Mkafuzu kwa uzuri.

Zaidi ningependa kuunga mkono Hoja ambayo iko mbele yetu hii leo. Kwanza, niipatie kongole Kamati ya Ugatuzi, Utumishi wa Umma na Majanga inayoongozwa na ndugu yangu Mheshimiwa Zia. Zaidi pia, Hoja ambayo inaratibishwa ni kuhusu shamba; nilikuwa nimeweka hapa Hoja kuhusu ile iliyopita na ningependa kutoa hiyo changizo kidogo wakati nikichangiza na hapa …

The Speaker (Hon. Mwambire): Ni vizuri kwenda na majira na itakuwa ni makosa …

Hon. Oscar: Ndiyo ndiyo….

The Speaker (Hon.Mwambire): Na itakuwa ni makosa kumvua….

Hon. Oscar: Nitakuwa wa haraka, mheshimiwa Spika…

The Speaker (Hon.Mwambire): Endelea na ile ambayo iko kwa sasa.

Hon. Oscar: Kwa sasa ningependa kuipongeza Kamati ya mashamba ambayo imeipitisha Kamati hii ya Manuspaa ya Malindi kwa kazi ambayo wameifanya.Wale ambao wako pale wana tajriba nzuri kulingana na Kamati ingawaje sijapata Ripoti; mimi sina haja ya kupinga hili. Kazi waliyopata ni kazi ambayo inafaa watumikie watu wa Kilifi. Yale majanga tuliyopata zamani vijana kukosa ajira, wengine kupata ajira hawalipwi, ningependa hizi Kamati ambazo zimeundwa ziende zikazingatie mambo hayo.

Vile vile, alivyotolewa kwa Mwenyekiti na Bodi yote ya Utumishi wa Umma ya kwanza ndivyo ambavyo vitafanyika kwa mtu yeyote ambaye atakuwa anakaidi yale matakwa ya watu wa Kilifi. Nimesimama, kuunga Hoja hii. Asante sana.

The Speaker (Hon. Mwambire): Mheshimiwa Betty, mheshimiwa Oscar amesema ni mdogo zaidi.

Hon. Oscar: Aliyechaguliwa kwa kura…

(Laughter)

Hon. (Ms.) Betty: Asante, mheshimiwa Spika. Kwa manufaa ya wanafunzi wa Kizurini, naitwa mheshimiwa Betty Kache na ninawakilisha vijana katika Kaunti yetu ya Kilifi. Mheshimiwa Oscar amesimama akasema yeye ndiye mheshimiwa mdogo kiumri kwa wale ambao walichaguliwa kwa kura. Kwa ujumla hawa wote ambao wako hapa mimi ndio kitinda mimba wao. Nina waheshimu, nawapenda na tunafanya kazi pamoja.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

(Applause)

Hon. (Ms.) Betty: Mulio hapo juu nyinyi ni dada zangu na kaka zangu. Kwanza ningetaka kuwambia hongera kwa kufika hapa. Mimi Betty Kache nikiwa hapa ndani nawakilisha vijana wa Kilifi na nyinyi hapo ni vijana. Kumekuwa na utata ya kuwa vijana ni nani. Wanasema kijana ni miaka kumi na minane (18) lakini mimi ningetaka kupinga. Kijana inaanzia kumi na tano (15) hadi thelathini na tano ama arobaini na tano (35-45) kama sijakosea.Ukiingia kwenye mitandao hilo utalipata…

The Speaker (Hon.Mwambire): Mheshimiwa, huwezi enda nje ya Katiba vile inatakikana…

Hon. (Ms.) Betty: Mheshimiwa Spika, sijaenda nje ya Katiba hata ukiangalia nimekuwa katika hiyo mada nikiongelea kuhusu kijana ni nani. Nimeingia katika mitandao na nikaangalia; pengine mitandao inatudanganya lakini hawa walio hapa wengi ni vijana.

The Speaker (Hon. Mwambire): Unajua mheshimiwa, ukileta huu mjadala utawakanganya kwa sababu hiyo iko katika dini fulani na pia Katiba imeweza kuweka ni miaka 18 hapa Kenya.

Hon. (Ms.) Betty: Mheshimiwa Spika, …

The Speaker (Hon. Mwambire): Hawa ni wale ambao wataenda kutahiniwa. Wacha nikupatie mfano; kwa wale wanasoma historia wanaambiwa kwamba waingereza walikuja wakaondoa ile utawala wa kimabavu ama ile iliyokuwa inaitwa uuzaji wa watu, lakini ukiangalia walivyokuja kuanzisha mashamba hapa Kenya wakachukua watu wetu na kuwafanyisha kazi kwa mashamba. Hawakuja kuondoa utawala wa mabavu walikuja kutugandamiza zaidi kwa manufaa yao.

Kwa hivyo, kuna mambo mengine ukiangalia yalivyonakiliwa katika vitabu na ukweli vile iko ni tofauti. Ni vyema kuenda vile ambavyo iko kwa manufaa yao hususan katika masomo. Itakuwa ni makosa wanafunzi wetu kutoka mwambao wa Pwani hasa Kizurini halafu waanze kunakili mambo tofauti ambayo itafanya pengine wasifaulu hatika somo la Kiswahili. Kwa hivyo, ningeomba mheshimiwa ubane tu pale kwenye Katiba inavyosema hapa Kenya na uendelee; usiangalie kwa umbo, tunaangalia kwa umri.

Hon. (Ms.) Betty: Asante, mheshimiwa Spika, kwa kuelezea kwa kina. Vile vile, ningetaka kubaki hapo kuwa walio hapa leo ni vijana na mimi kama Mwakilishi wenu nina wawakilisha vilivyo. Mimi kitu ambacho nataka niwambie ni kuwa mnaenda kukalia mtihani wenu wa mwisho ambao mtaufanya hivi karibuni; msiwe na uoga na kubabaika kwa sababu mmesoma kwa miaka minne na ni siku tu za kuhesabu na hizo siku hizo ndo zitakwambia kuwa wewe ni kitu gani unakitaka katika maisha.

Mimi Betty, ninacho waomba ndugu zangu, baada ya miaka mitano ama hata kumi tuwe wengi katika Bunge la Kaunti na hata katika Bunge la Kitaifa kule juu. Kwa sababu, miaka inavyoenda pia mimi sitabaki hapa. Nataka kupanda zaidi na hata muwe mnaniona kule kwa Bunge la Kitaifa. Kwa hivyo, nyinyi nanyi nawaomba muwe na hiyo ari ya kuwa viongozi kwa sababu Kilifi Kaunti inataka viongozi wengi zaidi na zaidi na uongozi wa sasa ni uongozi wa vijana. Kwa hiyo, karibuni sana na MCA wenu ambaye ni mheshimiwa Birya ni Mwenyekiti wangu kwa Kamati ya *Finance* na mimi ndiye mwanachini wake. Kwa hivyo, nyinyi ni watoto wetu ikiwa baba yenu ni Mheshimiwa Birya Fondo.

(Laughter)

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Speaker (Hon.Mwambire): Kwa hivyo, umekubali si vijana ni watoto? Endelea.

Hon. (Ms.) Betty: Mheshimiwa Spika, nataka kuunga mkono Hoja hii ya leo kuhusiana na mambo ya *Municipality*. Vijana wengi wamekuwa wakililia mambo ya ajira. Ni kweli ajira imekuwa ni shida; kuna mambo tofauti tofauti ya kuudhi na kuumiza moyo ambayo yamekuwa kule nje.Vijana wamekuwa wezi, wameingilia mambo ya mihadarati na pia wameingilia swala la ushoga na usagaji. Haya mambo yanafanyika kwa sababu hakuna ajira na kila mtu anataka kuishi yale maisha ambayo anayatamani.

Kwa hivyo, wale wote ambao wamepata nafasi ya kuwakilisha watu wa Kilifi katika hii bodi, tungelitaka kuwambia kuwa watu tumewaamini ndio maana leo hii tumewapitisha katika hili Bunge. Nasi tutafanya yale ambayo yanastahili na hao wafanye majukumu yao kama inavyopaswa.

Mheshimiwa Spika, nasimama tena kuunga mkono Hoja hii na nawatakia kila la heri katika kazi yao mpya na katika ofisi zao ambazo wataenda kuanza hivi karibuni. Asante.

Hon. Rashid: Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii. Nachukua fursa hii kuwashukuru walimu waliohakikisha ya kwamba wanafunzi wa kidato cha nne wamefika katika Bunge hili ili kupata elimu katika lugha ya Kiswahili.

Bw. Spika, kabla sijasema kama naunga mkono au la, nitakuwa ni mwizi wa fadhila kama sitawakaribisha na kuwapa nasaha wanafunzi walioko hapa maana mimi pia ni mwalimu na gwiji wa lugha ya Kiswahili.

Nimesikiza kwa umakini wazungumzaji waliotangulia. Katika kuzungumza kwao nikakumbuka katika katibu cha fasihi kwa jina anwani “Siku Njema” mhusika mmoja kwa jina Kongowea Mswahili nikinukuu “Kinywa chako mwendani kisikusifu ngoja sifa upewe.” Naona wenzangu wamekaidi maneno haya. Niko kwenye Bunge hili kama mwalimu naweza nikakubaliana nao kwa sababu ni fasihi; wengine wamesema wao ndio wadogo kabisa. Wanafunzi mliofika hapa mimi ndiye Mheshimiwa Rashid Odhiambo, Mheshimiwa wa Malindi *Town Ward*, mheshimiwa ambaye amechaguliwa na kura nyingi kabisa katika Bunge hili.

(Laughter)

Nasaha yangu ambayo ningewapatia wanafunzi; nina imani ya kwamba jambo muhimu sana liliowaleta ni kupata misamiati ya Bunge. Ninawaomba mchukue misamiati ya Bunge na mambo mengine msiyachukue kama yalivyozungumziwa kwa sababu wengi waliokuwa wakizungumza kwa lugha ya Kiswahili sio katika taaluma zao. Mkiangalia hawakuzingatia katika maswala ya fonolojia, sintaksia na semantiki, hawakuyazingatia. Kwa hivyo, kile ambacho ningependa kuwaomba yale ambayo mmeyapata mtakaa chini na walimu wenu na myapige msasa. Najua wengi hawatakubaliana na mimi lakini mwalimu wenu amewafundisha akiwaambia cha mkufuu mwanafuu ha, akila hu, cha mwanafuu mkufuu hu akila ha.

(Laughter)

Na mwisho, nawarudisha katika semi. Kitabu cha ‘Siku Njema’ aliposema “mgomba changaraweni haupandwi ukamea”. Wacha nichukue fursa hii baada ya kuwapatia nasaha wanafunzi waliofika hapa kwamba naunga mkono Hoja hii ambayo iko mbele yetu na vile vile naomba waheshimiwa wenzangu ambao wamebakia waunge mkono Hoja hii kwa sababu ni haki ya kidemokrasia ya kila aliyeko hapa kutoa uamuzi wake. Asanteni na Mungu awabariki.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

(Applause)

The Speaker (Hon. Mwambire): Huyo ni mheshimiwa mwalimu Rashid Odhiambo. Mheshimiwa Umi Abu.

Hon. (Ms.) Umi: Asante, sana mheshimiwa Spika. Asante kwa kunipa nafasi hii. Ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha hapa siku ya leo. Vile vile, kwa manufaa ya wageni ambao wako kwenye Bunge hili tukufu, kwa majina naitwa Mheshimiwa Umi Abu Mohammed *a.k.a* mama lao *a.k.a big* mama.

(Laughter)

Nimesimama kuunga mkono Ripoti hii. Niipongeze Kamati mmoja wao nikiwa mimi kwa kazi nzuri waliyoifanya.Wamekaa kwa weledi na fahamu zao. Mimi nikiwa mwanafunzi wa Kiswahili ambaye sijahitimu, maana mheshimiwa ambaye amekuwa kwa Sakafu ni mwalimu na mimi nitakuwa mwanafunzi wake. Mimi ningetaka kuwapongeza wale ambao tumewafanyia *vetting*. Niwaambie wawe na safari nzuri na wachukue mifano ya wale wengine ambao wameweza kufanya vizuri. Vile vile, nikiwaachia msemo wa kuondoka niseme tusitoke kufiwako tukaenda kuliwako nyama. Kwa hivyo, wawe mfano wafanye kazi vizuri tusaidie watu wa Kilifi. Asante, Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Mwambire): Mheshimiwa Paul Charo Kitsao.

Hon. Paul: Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii. Kwanza, kwa wanafunzi ambao wametutembelea kwa manufaa yao, kwa majina mimi naitwa Mheshimiwa Paul Charo, natoka Wadi ile ya Magarini ambako ukivuka tu daraja la Sabaki, kuna matikiti maji pale. Namuomba mwalimu ambaye anahusika, siku moja awatembeze. Kuna viboko pale chini ya mto halafu kuna haya matikiti maji matamu sana. Nataka nishukuru vile ambavyo mmekuja rafiki yangu Mheshimiwa Birya Fondo akiwa ni rafiki yangu wa karibu sana. Pia, kwa sababu shule ile ya Kizurini ni shule ya upili, si ajabu kuna wengine wametoka wadi mbali mbali, hata kuna uwezekano wengine wametoka sehemu hizo za Magarini. Langu tu ambalo nataka niwajuze ni kwamba mfanye bidii, mzingatie masomo maana masomo ndiyo ambayo yatafanya maisha yako yawe vizuri.

Mheshimiwa Spika, singependa kuongea maneno mengi. Langu ni kuunga mkono mia kwa mia Kamati ambayo ilisimama na kuuliza maswali wale watahiniwa ambao ni halmashauri ya Bodi ya Malindi ilifanya kazi nzuri sana.

Pia, nimenukuu yale yote ambayo yameandikwa hapa; hawakuangalia tu maeneo fulani peke yake bali waliangalia sehemu tofauti tofauti na kabila tofauti tofauti na naona hakukuwa na upendeleo. Nimeona mmoja wao kati ya wale ambao wako pale anatoka katika maeneo yangu; ijapo anaishi Malindi lakini ukoo wake uko sehemu ile ambayo natoka. Wacha niipongeze Kamati nzima.

Wanapoanza kazi, nasema ya kwamba wafanye kama vyenye Kamati haikuwa na ubaguzi wowote. Kaunti yetu ya Kilifi ina matatizo mengi; vijana wengi hawana vibarua. Wanapoingia pale wafanye kazi kwa uzuri bila upendeleo wala ubaguzi ili vijana wetu wapate vibarua na maisha yaendelee vizuri ili tuendelee kuijenge Kilifi yetu. Kwa hayo mengi au machache, naunga mkono na tuwe na mchana mwema.

(Question, that the Mover be now called upon to reply, put and agreed to)

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Ray: Asante, mheshimiwa Spika, kwa kunipatia fursa hii tena. Naanza kwa kupongeza waheshimiwa wenzangu kwa kuchangia Hoja hii ya uteuzi wa Halmashauri ya Manuspaa ya Malindi. Ningeomba waheshimiwa wenzangu waweze kupitisha majina haya sita kwa sababu pia utendajikazi hapa Malindi uko na shida. Mamlaka yote yalikuwa yamepewa Meneja peke yake ambapo haitakuwa sawa kwa utendajikazi kwa sababu hawezi fanya kazi zote yeye mtu mmoja.

Kikatiba, kuna kazi ambayo yatakikana wanachama wa bodi wafanye uamuzi. Sasa, kufanya uamuzi yeye binafsi halafu kuwe na shida baadaye itakuwa si vizuri kumsumbua Meneja kwa malengo ya kuhakikisha mji wa Malindi uko sawa kimaendeleo, usafi, mpangilio wa mji; kila kitu kitategemea kamati hii ambayo tutaipitisha hapa leo. Ninasema shukrani na nina imani na nyinyi kwamba mtapitisha hivi leo angalau Malindi kuwe kuna Bodi ya kuweka uamuzi wa maendeleo. Asante.

(Question put and agreed to)

ADJOURNMENT

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Members, we have come to the end of today's session. As usual, before we adjourn, I know you will be notified through notice on the next sitting. May you have a good day.

The House rose at 11:49 a.m.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*